BINT EL SUDAN
Perfume • Powder
Pomade • Deodorant

MARASHI
ASILI YA MAPENZI
HAKIKA
UTA FURAHI

Wasafishaji mashuhuri wa picha za rangi za *FUJI* ulimwenguni sasa wanapatkiana njini Mombasa

Aina zote za picha za rangi zinachapishwa:

FUJI • KODAK • AGFA
SAKURA • COLOURAMA

KWA USAFISHAJI WA PICHA ZAKO ZOTE ZA RANGI HAKIKISHA UNAZITUMA KWA MITAMBO MIPYA YA KISASAS YA FUJI

Zungumza na *Riaz Alibhai* kwa simu 313589, Mombasa ama fika kwenye mitambo hiyo mipya ya *FUJI*, iliyo pakana na afisi ya *Coastweek*, gorofa ya kwanza ya jumba la Banki ya Grindlays, katika barabara ya Digo Road na Nkrumah road.

Vitanda Vichache Hospitali

NATOA ombi kwa Serkali yetu tukufu chini ya Mtukufu Rais Daniel Arap Moi ifanye taratibut za kurekebisha hali ilivyo katika hospitali Kuu ya kuzalia ya akina mama ya Coast General iliyoko mjini Mombasa.

Hakika hali mbaya iliyoko sasa inasikitisha hasa kuona akina mama wakilalal kitanda kimoja wanawake wawili. Wanawake waliojifungua wanastahili nafasi ya kutosha baada ya kujifungua ama kabla ya kujifungua.

Kuwalaza wanawake wawili pamoja ni shida kwani wengine huwa wazito na hata mara nyingine wengine hujiamulia kulala chini badala ya kulala juu ya kitanda kutokana na taabu aliyonayo mwenzake.

Natoa ombi kwa Wajumbe Wabunge na Madiwahi wa Mombasa washirikiane bega-kwa-bega katika kutatua matatizo ya mji huu na wafuate mfano wa Wajumbe wa Taita-Taveta wanavyoshirikiana na kuweza kutatua matatizo yao.

Nachukua fursa hii pia kumshukuru Mtukufu Rais Daniel Arap Moi kwa uamuzi wake wa kumchagua Bw. Noah Katana Ngala kama Waziri wa Habari na Utangazaji. Tunamuombea Bw. Ngala kila laheri, baraka na umri mrefu.

MNYIKA M. MWAIGHO,
MOMBASA.

HII NI TIMU moja ya vijana ambayo inafanya maendeleo mazuri katika Mombasa. Hawa ni watoto wa Kaloleni wanaojulikana kama "Chelsea FC" ambao wanacheza mchezo wao wa mwisho leo Ijumaa dhidi ya timu ya Posta. Waliosimama ni Hemed Nassor "Chaguga", Ayoub, Kenyatta, Ali Bakari, Suleiman Nassor "Suche", Abdulkarim "Amba" na Lumumba. Waliochutama ni Anwar Mbarak, Gordon, Ali Khamis, Hassan Kandindo, Hamdo, Muryoki na Breik Yislam.
PICHA: SALIM BAHANNAN

'Hatuvunji Timu Yo Yote' — Asema Sheriff Nassir.

na Abdulrahman Sheriff

MAKAO Makuu ya Chama kinachotawala cha *KANU* wilayani Mombasa kimetangaza rasmi kwamba kutakuwako na timu ya mchezo wa soka itakayojulikana kama *Kanu Mombasa FC;* timu ambayo itawakilishwa na wachezaji kutoka Wadi zote 24 za Wilaya ya Mombasa; wachezaji wenye maarifa na ujuzi wa kutosha wa kulisakata kabumbu la hali ya juu!!

Penedekezo la kuanzisha kwa timu hiyo ya Mseto ya *KANU* lilipitishwa kwa kauli moja kwenye Mkutano wa Viongozi wote wa Wadi 24 wa chama cha *KANU* wilayani, viongozi wa Kanu katika matawi madogo ya Mombasa Kusini, Magharibi, Kati na Mashariki uliofanyika kwenye Ukumbi wa Waislamu wa Sakina ulioko Majengo. Hakuna hata mjumbe mmoja aliyepinga azimio hilo.

Mkutano huo chini ya Mwenyekiti wa *KANU* wilayani Mombasa, Sheriff Nassir ulipitisha kwa kauli moja kuwa *KANU*, ikiwa ndicho chombo cha pekee nchini kuona wanamichezo wanajiendeleza na kuinua hali ya michezo nchini, lazima kifanye taratibu maridhawa za kuona maendeleo ya michezo yanapatikana katika kila sehemu ya Kenya.

"Hapana shaka uamuzi huu wetu wa kufungua timu ya *Kanu Mombasa* utasaidia sana kurudisha hadhi ya mchezo wa mpira katika Mombasa na Pwani nzima kuwa kama hapo zamani wakati mkoa wetu ulikuwa ukitowa Wanasoka wengi kuwakilisha Taifa letu katika mashindano ya Kimataifa dhidi ya Mataifa mengine katika Afrika Mashariki na Afrika nzima". alisema Bw. Nassir katika mahujiano na COASTWEEK.

UAMUZI huo wa KANU huenda umezishtua timu nyingi za hapa Mombasa kwamba pengine wachezaji wake wazuri watataifishwa na timu hiyo ya KANU lakini Bw. Nassir alivihakikishia timu zote za Mombasa kuwa visiwe na wasiwasi kwani timu hiyo itakuwa ikicheza mechi za kiratiki pamoja na kufanya ziara ya kutembelea kote nchini na nchi nyingine pekee!

Akifafanua zaidi, Bw. Nassir aliye pia Mbunge wa Mombasa ya Kati na Waziri Mdogo wa Ardhi na Makao alisema kuwa timu hiyo itakuwa ni ya Kombaini ya Mombasa na itakuwa ikipambana na timu za mikoa mingine kwa michuano ya kirafiki ama ya kugombania vikombe fulani na itasimamiwa na Viongozi wanaoendesha Soka katika Pwani yaani (Shirikisho la Soka nchini (K.F.F.) tawi la Pwani.

"Hakuna timu itakayopokonywa mchezaji wake yoyote na wala si nia ya *KANU* kuona mageuzo ya mfumo wa uendeshaji wa soka mkoani lakini twataka wachezaji wetu mahodari wapate ujuzi zaidi ya kulisakata soka watakapotembelea nchi nyingine, kuona na kupata ujuzi wa wenzetu kote ulimwenguni", alisema Bw. Nassir na kuengeza kuwa baadaye wachezaji wetu watanufaika na kurudisha tena hai njema ya soka mkoani.

BW. NASSIR

Timu hiyo ya *KANU*, habari za kuaminika zinaeleza, tayari ina nguo ama mavazi rasmi yenye alama ya Jogoo iliyo pia alama ya chama cha *KANU* na rangi za nguo zake ni kama zile za bendera ya chama. Wadadisi wa soka wanaona kuwa timu hiyo itawafanya wateuzi wa timu ya Harambee Stars wanawaona kila wakati wanasoka wa Pwani na huenda wakawateua kwenye Timu ya Taifa.

Katika mkutano huo, mjumbe wa *KANU* katika wadi ya Kisauni (Mwanamama) alisimama kwa nidhamu na kuwaambia wajumbe wenzake: "hakika ni jambo la furaha kuona *KANU* imeonelea umuhimu wa michezo na kwa niaba ya akina mama, napenda kupendekeza kuwa timu ya Netboli ya KANU ya akina mama ianzishwe pia kuinua hali ya mchezo huo katika Mombasa.

Bw. Nassir alikubaliana na pendekezo hiko na akamfahamisha mjumbe huyo kuwa KANU ITAFANYA TARATIBU PIA ZA KUANZISHA TIMU YA Netboli kwa manufaa ya akina dada na akina mama wanaopenda na wenye nia ya kuendeleza mchezo huo. "Kuna mashindano ya Netboli kwa timu za Afrika Mashariki na Kati na kwa hivyo mchezo huo pia ni muhimu" akasema Bw. Nassir huku akishangiliwa na wajumbe waliokuweko mkutanoni.

Nampongeza N. Katana Ngala

NAPENDA kutoa shukrani nyingi kwa Mtukufu Rais wetu Mpendwa Daniel Toroitich Arap Moi kwa uamuzi wake wa kumpandisha cheo aliyekuwa Waziri Mdogo katika Afisi ya Rais, Mhesimiwa Noah Katana Ngala kuwa Waziri Kamili.

Hakika uamuzi huo umewafurahisha Wapwani wote kwa Mheshimiwa Ngala ameinukia kuwa kiongozi mwenye busara na hekima na uteuzi wake kama Waziri wa Habari na Utangazi umekuwa wa maana sio kwa Wapwani pekee bali hata kwa Wakenya wote.

Ningependa waziri huyo mpya wa habari na utangazaji afanye bidii kuturudishia Idhaa ya Pwani ambayo kwa hivi sasa haisikiki tena mitamboni. Tunamuomba atufanyie hivyo.

ABDULRAHMAN BAFADHIL, TAKAUNGU

Farucci

BINT EL SUDAN
Perfume • Powder
Pomade • Deodorant

MARASHI
ASILI YA MAPENZI
HAKIKA
UTA FURAHI

JISHINDIE VIATU MARIDADI VYA FARUCCI KWA MSHINDI WA KWANZA NA 'BINT EL SUDAN - GIFT PACK' KWA MSHINDI WA PILI NA WATATU ATAPATA ZAWADI YA FLANA YA FARUCCI

CROSSWORD No. 218

KWENDA KULIA:

1. Vitu au vyombo vinavyokwenda kwa magurudumu. 4. United Kingdom. 6. Kujikwaa, 8. Hufanya barabara kuwa imara. 9. Twavumbua. 12. "Hiana" imepungua herufi moja. 14. Kiungo cha maneno. 15. Kivazi cha kiume. 16. Hafifu, yenye thamani ndogo. 17. Keti. 18. Kipande cha mti cha kupikia.

KWENDA CHINI:

1. Majani ya mnazi. 2. Angalia, tazama. 3. Ni kiwanja maarufu cha Kandanda Dar-es-Salaam. 5. Bandari mashuhuri Afrika Mashariki. 7. Tamko la kukataa. 10. Kinyume cha konda. 11. Ananyonga. 13. Ukubwa. 15. Hamu ya maji.



MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO No. 217

KWENDA KULIA: 1. MASHAIRI, 5. NSO, 6. LAITI, 8. ABIRIA, 11. WAUME, 13. URU, 14. KUBALI, 15. KA, 16. ANA, 18. LAMU, 21. IF, 22. AELEWA. *KWENDA CHINI:* 1. MALAWI, 2. HATAMU, 3. RN, 4. ISHIRINI, 7. IBEBE, 9. RULA, 10. AU, 12. UKAME, 15. KAA, 17. AFU, 19. UL, 20. CW.

WASHINDI WA FUMBO LA KUJAZA MANENO No. 217.

1. ESHA A. AHMED, Sanduku la Posta 86876, Mombasa, 2. Mrs. Jane Wugimbi, Sanduku La Posta 90581, Mombasa, 3. J. Chalala Sanduku La Posta 85696, Mombasa.

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:—

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa. Kila baada ya wiki mbili, Mshindi wa kwanza atapata viatu maridadi vya Farucci; wa pili atapata 'Bint El-Sudan-Gift Pack' na watatu atajinyakulia flana ya Farucci. Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK* Limited Mombasa. Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa Mhariri *COASTWEEK*, S. L. P. 87270, Mombasa. Mwisho wa kutuma majibu na jumatano, September 18, 1985 saa, nne asubuhi.

JINA...

SANDUKU LA POSTA.............................